



Transparency & Accountability for the Extractive Industry

HakiRasilimali
P.O. Box 38486, Dar es Salaam
Mobile: +255 745 655 655
Email: info@hakirasilimali.or.tz
Web: <http://www.hakirasilimali.or.tz>

Publish What You Pay
Tanzania

TAARIFA KUTOKA KWENYE MKUTANO MKUU WA ASASI NA AZAKI KATIKA KUANGALIA FURSA ZITOKANAZO NA SEKTA YA MADINI MAFUTA NA GESI, KWA MAENDELEO YA NCHI

St. Gasper Dodoma Kuanzia Tarehe 2 - 3/11/2017

HakiRasilimali – Publish What You Pay Tanzania, ni jumuiko la asasi za kiraia zinazoshughulikia ushawishi wa sera katika sekta ya uziduaji nchini.

Ni kawaida kwa kila mwaka HakiRasilimali-PWYP Tanzania waaandaa mkutano wa kitaifa na wadau mbalimbali kutoka nyanja zote ndani na nje ya Tanzania, kwa kusudi la kujadili, kujifunza na kushirikishana uzoefu kataika utetezi na ushawishi wa michakato ya maamuzi yatokanayo na sekta ya uziduaji ili kuleta maendeleo endelevu yanayotarajiwa na sekta hii kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

Kwa mwaka 2017, mkutano huu ulidhamilia kuwakutanisha tena wadau wa sekta ya uziaduaji ili kujadiliana, kushiriki na kujifunza kutoka kwa Serikali, makampuni, asasi/azaki ,waandishi, jamii na wasomi kwa jinsi gani usimamizi wa rasillimali za madini, mafuta na gesi asilia unaweza kuwa chachu ya maendeleo Tanzania.

YALIOJIRI

Ushiriki wa wananchi:

Kwanza ifahamike na kutambulika kwamba Rasilimali za nchi ni za wananchi kwa mujibu wa katiba. Hivyo wananchi wana haki ya kushiriki kikamilifu na kwa muda muafaka katika maamuzi mbalimbali yenye kuleta tija katika sekta ya uziduaji. Na serikali ni wakala anayesimamia kwa niaba ya wananchi.

Jukumu la Bunge

Bunge linatakiwa kuwa huru katika kusimamia serikali kwenye usimamizi wa rasillimali za nchi hususani maamuzi yanayohusu maendeleo endelevu ya sekta husika. Maamuzi hayo

yanatakiwa kufanyika kwa kuzingatia ueledi na maslai ya taafa na si kiitikadi. Ili kufaniklisha hili, kunahaja ya wabunge kujengewa uwezo zaidi, katika kuelewa taratibu zihusuzo sekta ya uziduaji madini, mafuta na gesi asilia.

Kuongeza uhuru wa kamati za Bunge kupitia maboresho ya kanuni katika kusimamia sekta ya nishati na madini. Pia kurudisha vifungu vya sheria vinavyotoa mamlaka kwa bunge kupitia na kuridhia mikataba yote kati ya serikali na makampuni mbali mbali.

Lakini kwa upande mwingine, Bunge kwa kushirikiana na serikali, linajukumu la kuhakikisha sheria zinazotungwa hazikinzani wala kuzuia utendaji kazi kikamilifu wa taasisi zingine kama, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Nafasi na mianya iliyopo katika sharia imekua ikitumika na makampuni makubwa ya uchimbaji katika kukwepa kodi.

Sera na sheria

Nimuhimu kwa mihimili yote mitatu ya serikali kuhimiza juu ya utekelezaji wa sera na sharia zile zinazoonekana kuwa na manufaa katika nchi. Nimuhimu kwamba hatua za utekelezaji wa sera na sheria zikaambatana na utoaji wa taarifa sahihi kwa wananchi wakiwemo wadau kama AZAKI na mashirika binafsi kwa wakati sahihi. Hali hii itatoa muda wakutosha wakuzitafsiri, kuzielewa na ikiwezekana kutoa maoni kwa serikali kwaajili ya maboresho na ufanisi zaidi pindi sera na sheria hizi zitakapokua zikitumika.

Sambamba na hilo, imependekezwa kwamba ziandaliwe kanuni ili zisaidie kuondoa mgongano na mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria husika, ili kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa sheria ya mazingira. Mfano pale ambapo sheria inapaswa kutumika katika kusimamia au kutathmini mwenendo wa makampuni ya uchimbaji madini kabla na baada ya shuguli za uchimbaji, ili kujibu maswali yafuatayo (Je nikwakiasigani makampuni haya yanaruhusiwa kuharibu mazingira vikiwemo vyanzo vya maji na uoto wa asili? Na pia je, makampuni yana jukumu gani la kuboresha mazingira pindi yanapo maliza shuguli za uchimbaji?)

Jamii na usimamizi wa haki za kibinadamu

Miongoni mwa majukumu ya AZAKI katika nchi, ni kuendelea kuelimisha wananchi na jamii juu ya maswala yahusuyo maendeleo na ustawi wao, kwa lengo la kuongeza nguvu na sauti ya umma. Jukumu hili halipaswi kubezwa wala kudharauliwa kwani, linachangia katika kujenga jamii yenye uelewa na nguvu ya kuhoji mambo mbali mbali ya maendeleo ya sasa na yabaadae.

Mkutano huu uliona kwamba kuna fursa nyingi zinazoweza kujitokeza endapo serikali itatoa nafasi zaidi za ushirikiano na majadiliano yenye kuelimishana baina ya wamiliki wa migodi, wanao endesha shuguli za uchibaji mkubwa, wachimbaji wa kati, wachimbaji wadogo na jamii zinazo zunguka maeneo ya uzidua jadi madini, gesi na mafuta.

Miongoni mwa faida za kulifanya hili ni pamoja na kujenga mahusiano mazuri na yenye tija baina ya wadau wa sekta husika. Hii inamaanisha kujenga Amani na kupunguza misuguano inayoweza kusababisha ugonvi na kisha hasara za mali au watu kupoteza maisha katika maeneo ya migodi.

Lakini pia kwa kufanya hivi, itasaidia sana katika kuelimisha jamii juu ya uhalisia wa yatokanayo na hatua mbali mbali katika mnyororo wa thamani wa bidhaa zinazo zalistwa. Pia kufaham kijumla manufaa yanayoweza kupatikana kwa mtu mmoja mmoja atakae jishugulisha (mfano kupata ajira), kwa jamii inayo zunguka eneo la uzalishaji kuitia asilimia zinazotolewa halmashauri na serikali za mitaa na kwa taifa zima, kuitia makato ya kodi na mpango ya hisani. Hatua hii itasaidia kwenda kinyume na simulizi au nadharia potofu zinazojengwa na wanasiwa wasio waaminifu na wasio na taaluma ya uzalishaji wala ujuzi wa thamani ya bidhaa husika juu ya utajiri na faida za haraka haraka.

Sambamba na kutoa fursa za majadiliano, serikali inashauriwa kutoa nafasi kwa wananchi katika ngazi mbali mbali, kujadili na kutoa maoni juu ya rasilimali za nchi yao pasipo

vitisho. Nakisha iundwe mufumo yautoaji taarifa na mrejesho juu ya maamuzi yanayofanyika hususan kuhusu shuguli za uziduaji.

Maudhui ya ndani

Pia kunahaja ya kutoa nafasi zaidi kwa watanzania kujengewa uwezo ili wazitumie vizuri fursa zitokanazo na shuguli za uziduaji madini, mafuta na gesi. Kwa kutumia vyuo vya ufundii na vyuo vikuu vinavyo toa taaluma za utafiti, uziduaji na uongezaji wa thamani ili kushiriki kikamilifu, katika kusimamia na kufaidi matunda yatokanayo na shuguli za uchimbaji/uziduaji.

Pamoja na hilo, serikali hainabudi kuyatazama manufaa yatokanayo na shuguli za uzalishaji kisekta peke yake, bali inapaswa kuangali mafungamano na mahusiano baina ya taasisi na sekta mbali mbali. Hii itaboresha mgawanyo wa uwekezaji na kutotoa nafasi kwa sekta moja kuweza kunufaisha sekta zingine. Mfano sekta ya kilimo na sekta ya uchimbaji madini zinauwezo wakuzisaidia jamii, hususan jamii za wachimbaji wadogo katika kukuza vyanzo vyao vya mapato na kutoa ajira mbadala pindi uzalishaji unapopungua kwenye michimbo.

Hatua hii iambatane na kuwepo kwa viwango na tathmini za mchango/michango inaytolewa na makampuni ya uchimbaji kama sehemu ya jukumu lao kisheria, kwa jamii zinazo zunguka maeneo ya migodi/maeneo yenye shuguli za uchimbaji.

Mahusiano baina ya nchi wanachama wa Afrika mashariki Nimuhimu kufaham kwamba zipo faida nyingi zinazotokana na ushirika baina ya nchi jirani. Ili kujijenga na kuhakikisha kunaushindani wenyewe manufaa baina yetu na majirani zetu wa Kenya na Uganda, ilipendekezwa kwamba ni vyema kikaundwa chombo cha

pamoja ambacho kitashugulikia maswala ya maliasili na rasilimali ambazo zipona zinatumika baina ya nchi wanachama wa Afrika mashariki.



Transparency & Accountability for the
Extractive Industry

HakiRasilimali
P.O. Box 38486, Dar es Salaam
Mobile: +255 745 655 655
Email: info@hakirasilimali.or.tz
Web: <http://www.hakirasilimali.or.tz>

Publish What You Pay
Tanzania

Miongoni mwa mambo ambayo chombo hicho kitashugulikia ni kuweka uwiano wa bei/gharama za mauzo na bei za bidhaa zinazo zalishwa ndani ya inchi manachama. Mfano kusiwe na nafasi ya Tanzanite inayo zalishwa Tanzania iuzwe kwa bei mbaya nchini kenya na kufaidisha wafanyabiashara tena ambwao sio wazawa wa nchi wanachama.

Imeandaliwa na

Sekretarieti ya HakiRasilimali



Transparency & Accountability for the
Extractive Industry